



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA MAKAMU WA RAIS

**TAMKO LA WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA
MAZINGIRA), MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO (MB.) KUHUSU SIKU YA
KIMATAIFA YA HIFADHI YA TABAKA LA OZONI
16 SEPTEMBER, 2023**

Ndugu Wanahabari,

Tarehe 16 Septemba mwaka huu, Tanzania tutaungana na Jumuiya ya Kimataifa kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni kama kumbukumbu ya tarehe ya kutiwa saina Itifaki ya Montreal ya mwaka 1987 kuhusu kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni. Tabaka la Ozoni kazi yake kubwa ni kuchuja sehemu kubwa ya mionzi ya jua isifike kwenye uso wa dunia.

Ndugu Wanahabari,

Tabaka la Ozoni linapoharibiwa kuruhusu mionzi ya jua kufika kwenye uso wa dunia na hivyo kusababisha kuongezeka kwa magonjwa mbalimbali yakiwemo saratani ya ngozi, mtoto wa jicho, upungufu wa kinga dhidi ya maradhi na kujikunja kwa ngozi. Aidha, madhara mengine ni kuathirika kwa ukuaji wa mimea. Vile vile, baadhi ya kemikali hizi husababisha kuongezeka kwa joto duniani na hivyo kuchangia katika mabadiliko ya tabianchi.

Kemikali hizo ni kemikali/gesi zinazotumika katika majokofu na viyoyozi, vifaa vya kuzimia moto, usafishaji chuma, utengenezaji magodoro, ufukizaji wa udongo katika vitalu vya tumbaku na kilimo cha maua, hifadhi ya nafaka katika maghala na kadhalika.

Ndugu Wanahabari,

Kauli mbiu ya Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni mwaka huu ni **“Montreal Protocol: fixing the ozone layer and reducing climate change”** yaani **Itifaki ya Montreal: Hifadhi ya tabaka la ozoni na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi**” Kauli mbiu hii imechaguliwa kutokana na mafanikio ya kimataifa kupitia utekelezaji wa Itifaki ya Montreal katika kuchangia jitihada za kuhifadhi tabaka la ozoni na kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi.

Ndugu Wanahabari,

Tukiwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Kimataifa, kwa mwaka 2022 Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliadhimisha Siku ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni kwa:

- (i) Kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi tabaka ozoni na kuhamasisha matumizi ya kemikali ambazo ni rafiki kwa mazingira.
- (ii) Kutoa mafunzo kuhusu namna ya kudhibiti uingizaji wa kemikali nchini kwa Maafisa wa Idara za Serikali zilizopo katika Mpaka wa Namanga.
- (iii) Kutoa elimu kwa wanafunzi wa fani ya viyoyozi katika Chuo cha Ufundi Arusha pamoja na mafundi wa viyoyozi na majokofu kwa mkoa wa Arusha kuhusu namna bora ya kukarabati vifaa hivyo pasipo kuachia angani kemikali na hivyo kuharibu mazingira.

Ndugu Wanahabari,

Katika kuadhimisha Siku ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni kwa mwaka 2023, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu imepanga kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ambapo shughuli zifuatazo zimepangwa kufanyika:

- (i) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kupitia makala ya luninga kuhusu umuhimu wa kulinda tabaka la ozoni na kuendelea kuhimiza jamii kupunguza shughuli mbalimbali za kibinadamu ambazo zinasababisha mabadiliko ya tabianchi;

- (ii) Kutoa elimu kwa Chama cha Wanahabari wa Mazingira Tanzania (JET) na wahariri wa vyombo vya habari kuhusu umuhimu wa kulinda tabaka la ozoni; na
- (iii) Kutoa mafunzo kwa Maafisa Forodha na Wasimamizi wa Sheria waliopo katika Bandari ya Dar es Salaam pamoja na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuhusu namna ya kudhibiti uingizaji wa kemikali na vifaa vyenye kemikali zinazodhibitiwa na Itifaki.

Ndugu Wanahabari,

Nikiwa nahitimisha Tamko langu, napenda kutoa rai kwa kila mwananchi kushiriki katika kuhifadhi Tabaka la Ozoni na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- (i) Kuepuka kuingiza nchini gesi zilizopigwa marufuku na vifaa vinavyotumia gesi haribifu kama vile majokofu na viyoyozi vilivyokwishatumika (mitumba).
- (ii) Kununua bidhaa zilizowekwa nembo rasmi isemayo “*Ozone friendly*” au “low global warming potential” au yaani “sahibu wa Ozoni” au “uwezo mdogo wa kuchangia ongezeko la joto duniani”
- (iii) Kuepuka kutupa ovyo majokofu ya zamani ama vifaa vya kuzima moto vyenye kemikali zinazomong’onyoa Tabaka la Ozoni au kusababisha ongezeko la joto duniani.

Hivyo kupitia kwenu wanahabari naamini elimu hii itaendelea kutolewa kwa jamii ya Watanzania ili kuongeza ushuriki wao katika kutekeleza jukumu hili la kulinda sayari hii.

Nawatakieni maadhimisho mema ya Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni kwa mwaka 2023.

Asanteni sana,

Nawashukuru kwa kunisikiliza,

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....